**FAQs**

**VodaFibre ni nini?**

VodaFibre ni huduma ya intaneti ya nyumbani ya Vodacom inayotumia teknolojia ya FTTH (Fibre-to-the-Home). Huduma hii hutoa intaneti ya kasi na ya kuaminika moja kwa moja nyumbani kwako kupitia nyaya za fibre-optic VodaFibre inatoa kasi thabiti kwa ajili ya kutazama video mtandaoni, kufanya kazi au kusoma online, na kuunganisha vifaa vingi kwa wakati mmoja.

**Ni kasi gani zinapatikana?**

a. 50 Mbps
b. 75 Mbps
c. 100 Mbps
d. 200 Mbps

**Je, intaneti ina kikomo**

Ndiyo, intaneti haina kikomo, hivyo unaweza kuitumia bila kuwa na wasiwasi kuhusu matumizi ya data.

**Ninaweza kutumia faiba internet kwa nini / Faiba inafanyaje kazi?**

a. Fibre internet inaweza kutumika kwa kutazama video mtandaoni, kuvinjari, simu za video, kazi online, kucheza gemu, na kuunganisha vifaa vingi kwa urahisi.
b. Jinsi inavyofanya kazi: Faiba hutumia nyaya za ubora wa juu kupeleka intaneti kama mwanga moja kwa moja hadi nyumbani kwako, hivyo kupata muunganisho wa kasi na thabiti.

**Faida za VodaFibre ni zipi?**

kwako:
a. Furahia kasi kubwa na thabiti kwa streaming, browsing, na video calls
b. Unganisha vifaa vingi kwa wakati mmoja bila kupungua kwa kasi
c. changamoto ni chache kwa muunganisho wa kuaminika zaidi

**Tofauti kati ya Faiba na (intaneti za rauta) FWA ni ipi?**

Fibre hutumia waya unaounganishwa moja kwa moja nyumbani kwako hivyo kutoa intaneti ya kasi na thabiti, wakati FWA hutumia signal ya wireless kutoka kwenye nguzo ya karibu ambayo inaweza kuathiriwa na umbali au

**Je, Faiba inapatikana eneo langu?**

GPS location.
Ikiwa faiba inapatikana eneo lako, utaweza kuendelea na usajili.
Angalia upatikanaji hapa: https://vodafibre.vodacom.co.tz/

**Ninawezaje kuangalia kama eneo langu lina Huduma ya faiba?**

Unaweza kuangalia kama eneo lako lina huduma kwa kutembelea https://vodafibre.vodacom.co.tz/ na kuweka anwani ya nyumba yako au GPS location. Mfumo utaonyesha haraka kama VodaFibre inapatikana eneo lako.

**Nahitaji nini ili kujisajili VodaFibre?**

Ili kujisajili VodaFibre utahitaji:
a. Eneo ambalo VodaFibre inapatikana
b. Namba yako ya Vodacom
c. Namba yako ya NIDA
d. Barua pepe halali
e. Maelezo ya anwani ya nyumba yako
Hivyo ndivyo unavyohitaji kuanza.

C2 General

**Naweza kujisajili kwa kutumia namba yoyote ya simu?**

Bado hapana. Ili kujisajili VodaFibre utahitaji namba ya Vodacom kwani usajili unafanya kazi kwa laini za Vodacom pekee.

**Nataka kufunga huduma ya VodaFibre, nifanye nini?**

Ili kufunga huduma ya VodaFibre, tafadhali fuata hatua hizi:

a. Tembelea tovuti ya VodaFibre: https://vodafibre.vodacom.co.tz/

b. Angalia upatikanaji: Weka eneo la usakinishaji kwa kutumia anwani au GPS location kuthibitisha upatikanaji wa faiba
c. Chagua kifurushi: Kama faiba inapatikana, pitia vifurushi na uchague kinachokufaa.
d. Jisajili kama mtumiaji mpya kwa: Kuweka namba yako ya Vodacom; Kutoa jina na namba ya NIDA; Kuthibitisha namba kwa OTP; Kuongeza email na kutengeneza password; Kuthibitisha email kwa code iliyotumwa kutoka VodaFibre.
e. Kamilisha oda yako: Weka maelezo ya anwani ya nyumba yako, chagua tarehe ya ufungaji unayopendelea, na ukubali vigezo na masharti.
f. Endelea na malipo: Bofya “endelea na malipo” kulipia huduma.
g. Baada ya kukamilisha, mchakato wa ufungaji utaanza

**Ufungaji unachukua muda gani?**

Baada ya malipo kukamilika, ufungaji utafanyika ndani ya siku 5 kutoka tarehe yako ya ufungaji iliyothibitishwa, na huduma itakuwa

**Je, kuna gharama ya ufungaji?**

Hapana, hakuna gharama ya ufungaji wa VodaFibre.

**Nini hutokea wakati wa ufungaji?**

Wakati wa ufungaji, fundi wa VodaFibre atakuja nyumbani kwako kufunga waya za faiba, kuzipanua zinapohitajika, na kufunga routa ya Wi-Fi. Baada ya hapo, huduma itawezeshwa na kuwa tayari kutumika.

**Je, nahitaji kuwepo wakati wa ufungaji?**

Ndiyo, inashauriwa mtu awepo wakati wa ufungaji. Fundi atahitaji kuingia nyumbani kwako kufunga waya za faiba, kuzipanua inapohitajika, na kufunga routa ya Wi-Fi

**Rauta/ONT itawekwa wapi?**

mahali ambapo nyaya za faiba zinaingia na ambapo Wi-Fi hufuki ni nzuri zaidi. Fundi atakuongoza kuhakikisha kila kitu kimewekwa vizuri na kwa urahisi.

**OTP ni nini na kwa nini inahitajika wakati wa ufungaji?**

OTP (One-Time Password) ni namba ya usalama inayotumwa kwenye namba yako ya Vodacom au email iliyosajiliwa. Inatumika kuthibitisha utambulisho wako na kuwezesha huduma yako ya VodaFibre kwa usalama.

**Ni vifurushi gani vinapatikana?**

Tunatoa vifurushi vya VodaFibre vyenye kasi za 50 Mbps, 75 Mbps, 100 Mbps, na 200 Mbps

**Kila kifurushi kinagharimu kiasi gani?**

Bei za vifurushi vya VodaFibre ni:
a. 50 Mbps – TZS 75,000
b. 75 Mbps - TZS 100,000
c. 100 Mbps – TZS 130,000
d. 200 Mbps – TZS 240,000

**Je, kuna gharama nyingine za ziada?**

Hapana, hakuna gharama nyingine za ziada.

**Naweza kubadili kifurushi changu?**

Ndiyo, unaweza kuongeza au kupunguza kifurushi chako cha VodaFibre. Mabadiliko yataanza baada ya kifurushi chako cha sasa

**Je, kuna mkataba wa huduma?**

Hapana, hakuna mkataba. VodaFibre ni huduma ya kulipia kisha unatumia, hivyo unaweza kuendelea au kuacha baada ya kifurushi

**Ninawezaje kulipia kifurushi changu?**

Unaweza kulipia kurushi cha VodaFibre kwa kuingia kwenye akaunti yako ya VodaFibre na kutumia M-Pesa. Kutoka Account , Home page, nenda kwenye Top Ups, chagua kufurushi chako, kisha endelea na malipo. Baada ya malipo kukamilika, utapokea SMS ya

**Nitatozwa lini?**

Utatozwa unapofanya ununuzi wa kifurushi cha VodaFibre. Malipo hufanyika mapema, na huduma yako huanza kulingana na muda

**Nini hutokea nisipolipa kwa wakati?**

Usipolipa kwa wakati, huduma yako ya VodaFibre itasimama baada ya kifurushi chako cha sasa kuisha. Unaweza kurejesha huduma muda wowote kwa kufanya malipo ya kifurushi kipya.

**Ninawezaje kupata invoice statement?**

Kutoka Account, Home page, fungua sehemu ya Invoices. Utaona orodha ya invoice zote zinazohusiana na akaunti yako, chagua invoice yoyote kuitazama au kuipakua.

**Naweza kuruhusu malipo ya moja kwa moja ?**

Kwa sasa, malipo ya moja kwa moja haiwezekani. Utahitaji kufanya malipo mwenyewe kila kifurushi chako kinapoisha ili kuendelea

**Kwa nini intaneti yangu ipo taratibu?**

Intaneti kuwa taratibu inaweza kusababishwa na vifaa vingi vilivyounganishwa, matumizi makubwa, au changamoto za Wi-Fi nyumbani. Tatizo likiendelea, tafadhali wasiliana na watoa huduma ya VodaFibre : 100.

**Ninaweza kuunganisha vifaa vingapi?**

Rauta ya Wi-Fi inayotolewa na VodaFibre inaweza kuunganisha hadi vifaa 64 kwa wakati mmoja, hivyo vifaa vyako vya nyumbani vitaendelea kuunganishwa vizuri.

**Ninawezaje kuboresha mawimbi ya Wi-Fi nyumbani?**

Ili kuboresha mawimbi ya Wi-Fi nyumbani, weka rauta sehemu ya kati na wazi, na epuka vitu vinavyoweza kuzuia mawimbi. Kwa maeneo yenye mawimbi dhaifu, kutumia Wi-Fi extenders au access points kunaweza kusaidia kuongeza ufikiaji

**Hali ya hewa huathiri intaneti ya faiba ?**

Hapana, hali ya hewa kawaida haiathiri intaneti ya faiba. Hata kwa waya za fibre-optic za juu, VodaFibre hubaki thabiti na ya kuaminika katika hali za kawaida za hewa.

**Kasi yangu itakuwa sawa kila wakati na ile iliyotangazwa?**

Kasi za VodaFibre huwa karibu sana na kasi iliyotangazwa kutokana na muunganisho thabiti wa fibre. Tofauti ndogo zinaweza kutokea kulingana na matumizi ya Wi-Fi na idadi ya vifaa vilivyounganishwa.

**Nifanye nini kama sipati intaneti ?**

Kama hupati intaneti, kwanza angalia kama kifurushi chako hakijaisha. Ikiwa bado ipo , tafadhali wasiliana na watoa huduma kwa: piga 100.

C2 General

**Taa za rauta /ONT zina maana gani?**

Huu ni mwongozo rahisi wa taa za router/ONT:
a. Power – Kuwaka kunamaanisha kifaa kina umeme
b. PON – Kuwaka kunamaanisha faiba inafanya kazi
c. LOS – Kuzimwa ni kawaida; kuwaka nyekundu kunaonyesha tatizo la mawimbi ya faiba
d. WLAN – Kuwaka au kublink kunamaanisha Wi-Fi ipo active
e. LAN – Kublink kunaonyesha kifaa kimeunganishwa kwa cable
f. Intaneti – Kuwaka kunamaanisha intaneti ipo
Ikiwa LOS ni nyekundu au hakuna taa ya intaneti, tafadhali wasiliana na huduma kwa wateja wa Vodacom

**Ni wakati gani , napaswa kuwasha na kuzima rauta yangu?**

Unapaswa kuwasha na kuzima rauta yako kama intaneti ipo taratibu, haifanyi kazi, au baada ya kukatika kwa umeme. Kuzima na kuwasha husaidia kuweka huduma sawa na mara nyingi kurekebisha matatizo ya muda.

**Ninawezaje kuwasilisha tatizo?**

Unaweza kuwasilisha tatizo kwa kuwasiliana na huduma kwa wateja wa Vodacom: 100. Wapo tayari kusaidia kuangalia na kutatua matatizo ya huduma yako ya VodaFibre.

**Inachukua muda gani kutatua matatizo?**

Matatizo mengi hutatuliwa haraka iwezekanavyo baada ya kuripotiwa. Muda unaweza kutofautiana kulingana na aina ya tatizo, lakini watoa huduma wa Vodacom hufanya kazi kwa haraka kurejesha huduma yako.

**Ninawezaje kubadilisha neno la siri ikiwa nime sahau**

Kwenye login page, chagua nime sahau neno la siri na uweke email inayohusishwa na akaunti yako. Utapokea barua pepe yenye maelekezo ya kubadili neno la siri. Fuata link, kisha:
a. Tengeneza na kuthibitisha neno la siri jipya.
b. Weka OTP iliyotumwa kwenye barua pepe yako kuthibitisha mabadiliko
Baada ya hapo utaingia moja kwa moja kwenye akaunti yako

**Ninawezaje kuangalia kifurushi changu ?**

Unaweza kuangalia kifurushi chako kwa kuingia kwenye akaunti yako ya VodaFibre. Ukiwa umeingia, nenda kwenye Subscriptions → View plan ambapo utaona kifurushi chako kina isha muda wake lini.

**Ninawezaje kununua tena kifurushi changu ?**

a. Kutoka Account Home page, chagua Top Ups na uchague kifurushi unacho taka kununua tena.
b. Chagua top-up option, pitia summary, kisha endelea na malipo kupitia M-Pesa.
c. Baada ya malipo kukamilika, utapokea SMS ya kuthibitisha kuongezeka kwa muda wake
d. Unaweza kuangalia kita ishi lini muda wake kupitia akaunti yako

**Naweza kubadili taarifa za akaunti yangu?**

Ndiyo, unaweza kubadili taarifa za akaunti yako. Ingia kwenye akaunti yako ya VodaFibre na nenda kwenye My Profile ambapo unaweza kusasisha jina, barua pepe , namba ya simu, au kubadili neno la siri lako.

**Naweza kusimamisha huduma yangu kwa muda mfupi?**

Kwa sasa huwezi kusimamisha huduma ya VodaFibre. Hata hivyo, unaweza kuchagua kuto lipia tena kifurushi chako, na huduma itasimama moja kwa moja baada ya kifurushi cha sasa kuisha.

**Nini hutokea nikihamia eneo jipya?**

Kama ukihamia eneo jipya, unaweza kuomba VodaFibre kwenye anwani mpya kama faiba inapatikana huko.
Kifurushi chako cha sasa kita achwa kiishe, kisha utaweka ombi jipya kupitia akaunti yako ya VodaFibre. Baada ya malipo, ufungaji utaandaliwa kwenye nyumba yako mpya.

C2 General

**Ninawezaje kusitisha huduma yangu?**

Huhitaji kusitisha huduma ya VodaFibre. Hakuna mkataba, hivyo unaweza kuacha tulipia kifurushi chako na huduma itaisha moja kwa moja baada ya kifurushi cha sasa kuisha.

**Je, kuna gharama ya kusitisha?**

Hapana, hakuna gharama ya kusitisha. VodaFibre haina mikataba, hivyo unaweza kusitisha huduma kwa kutorlipia kifurushi chako.

**Nahitaji kurudisha rauta/ONT?**

Hapana, huhitaji kurudisha rauta/ONT. Mara baada ya kufungiwa, vifaa vitabaki nyumbani kwako hata kama huduma ya VodaFibre

**Nini hutokea vifaa vikiharibika au kupotea?**

Ikiwa vifaa vitapotea au kuharibika, tafadhali wasiliana na wahudumu wa Vodacom kwa msaada. Watasaidia kutoa msaada na kubadilisha kinacho hitajika ; hata hivyo, gharama za kubadilisha zinaweza kutumika kulingana na mazingira husika.

**OTP ni nini?**

OTP (One-Time Password) ni namba ya muda ya usalama inayotumwa kwenye namba yako ya Vodacom au email iliyosajiliwa. Inatumika kuthibitisha utambulisho wako na kuweka akaunti pamoja na huduma yako salama wakati wa kujiunga, kuingia, au

**Je, ninapaswa kushare OTP yangu na mtu yeyote?**

Hapana, hupaswi kushare OTP yako na mtu yeyote. OTP ni kwa matumizi yako pekee na husaidia kuweka akaunti na huduma yako

**Ninawezaje kulinda Wi-Fi yangu?**

Unaweza kulinda Wi-Fi yako kwa kutumia neno la siri lenye gumu na kuifadhi vizuri kwa siri. Epuka kutoa taarifa za Wi-Fi ili kusaidia kulinda huduma na vifaa vyako.

**Ni katika hali gani ninapaswa kuwasiliana na huduma kwa wateja?**

Unapaswa kuwasiliana na wahudumu wa Vodacom ikiwa huna intaneti, unapata matatizo ya kiufundi, au unahitaji msaada kuhusu akaunti, malipo, au vifaa. Piga 100.

**Je, kuna aplikeshi ya simu au tovuti ya kujihudumia mwenyewe?**

Ndiyo, VodaFibre ina self-service portal ambapo unaweza kusimamia akaunti yako, vifurushi, malipo. Aplikesheni ya simu, pia itapatikana kusaidia kusimamia huduma yako kwa urahisi zaidi.

C2 General